ewura

Energy and Water Utilities Regulatory Authority

Newsletter

January 2012

ISSN 1821 - 7273 TOLEO NA. 006

Mfumo wa Ununuzi wamafuta kwa pamoja waanza

Meli ya MT. ALPINE MONIQUE ikipakua shehena ya kwanza ya mafuta katika mfumo wa ununuzi wamafuta kwa pamoja kwenye eneo la kupakulia mafuta, Kurasini, Januari 2012.

Yaliyomo

Waraka wa Mhariri	Uk-3
Kutoka Dawati la Mkurugenzi Mkuu	Uk-4
Mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja waanza	Uk-5
Mafanikio ya kihistoria katika kuidhinisha bei	Uk-6
EWURA yasimamisha ujenzi wa vituo 25 kwa kukiuka masharti ya ujenzi	Uk-7
Ushiriki wa EWURA kwenye maonesho waimarisha kampeni ya elimu kwa umma	Uk-8
Wakurugenzi wa Bodi watembelea mamlaka za maji Kaskazini	Uk-9
EWURA: "Kazi yetu sasa inatambulika"	Uk-11
Rais apongeza uimara wa EWURA	Uk-13
Kamati ya Bunge yapongeza punguzo la tozo za mafuta	Uk-14
Uchakachuaji, uingizaji wa mafuta ya taa nchini wapungua	Uk-15
Matukio katika picha	Uk-16
Tanzia	Uk-19

BODI YA WAHARIRI

MWENYEKITI
Bw. Haruna Masebu

MHARIRI
Bw. Titus Kaguo

MHARIRI MSAIDIZI
Bw. Wilfred Mwakalosi

WAJUMBE
Bi. Miriam Mahanyu
Bw. Felix Ngamlagosi
Mhandisi. Charles omujuni

SEKRETARIETI
Bi. Hawa Lweno
Bi. Bi Janet Mwaipopo

OFISI YA EWURA
Ghorofa ya Sita, Harbour View Towers, Barabara ya Samora
S. L. P. 72175,
Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 - (22) 2123850/3/4/6
Nukushi: +255 - (22) 2123180
B/Pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: www.ewura.go.tz

Waraka wa Mhariri

Bw. Titus Kaguo

HERI ya Mwaka Mpya wapendwa wasomaji wetu! Kwa unyenyekevu wa hali ya juu nawakaribisheni katika toleo la sita la Jarida la Mamlaka ya Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ambalo ni la kwanza kwa mwaka 2012.

Nafarijika kuwakaribisha kusoma taarifa zetu kutoka katika sekta mbalimbali zinazodhibitiwa na EWURA. Kwa mara ya kwanza, Jarida hili linatolewa wakati Mamlaka ikiwa imepoteza wafanyakazi wake wawili mashuhuri, aliyekuwa Mkurugenzi wa Petroli, Bw. Siril Massay na Dereva Mkuu, Bw. Robert Nyirenda. Wasifu wa maisha yao wakiwa EWURA umeelezwa katika Jarida hili.

Wakati toleo la tano lilitoka muda ambao Mamlaka ilikuwa imeanza kuona matunda ya mfumo mpya wa kuweka vinasaba ili kudhibiti uchakachuaji wa mafuta na uuzaji ya mafuta ya nje ndani ya nchi na hivyo kukwepa kodi, toleo hili linatoka wakati Mamlaka imeanzisha mpango mpya wa Uingizaji wa Mafuta kwa Pamoja(Bulk Petroleum Procurement System-BPS), nchini Tanzania.

Kuwasili kwa shehena ya kwanza tarehe 4 Januari 2012, BPS inatarajiwa kuimarisha bei za mafuta na kuifanya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ikusanya mapato yake stahiki kutoka katika mazao ya mafuta.

Toleo hili, pamoja na kuchapisha Tanzia, pia linakuletea mambo mbalimbali ambayo EWURA imefanya katika kudhibiti kama vile, Kuanza kwa Uingizaji wa Mafuta kwa Pamoja, Umma waanza kutambua wajibu wa EWURA, Utafiti wa vituo vilivyojengwa bila vibali vya Mamlaka, Wajumbe wa Bodi watembelea Kanda ya Kasikazini, Jinsi EWURA ilivyoshiriki Maonesho mbalimbali, Uamuzi wa kihistoria katika bei za maji, Bunge lasifia kupunguzwa kwa tozo, kushuka kwa uchakachuaji kwaongezeka na habari kadha wa kadha.

Mnakaribishwa!

Kutoka Dawati la Mkurugenzi Mkuu

Bw. Haruna Masebu

Wapendwa wasomaji, nachukua fursa hii kuwatakieni kheri na mafanikio katika mwaka huu mpya. Kulingana na utamaduni wetu, makala zinazopatikana katika Jarida hili la toleo la sita zinajadili masuala yanayohusiana na mamlaka yetu katika kuendeleza na kulinda maslahi ya wadau katika sekta za nishati na maji.

Mwanzoni mwa mwaka 2011, EWURA ilianzisha mfumo mpya wa kufanya mapitio ya bei kwa mamlaka mbalimbali za maji Tanzania Bara na hivyo kuwezesha udhibiti wa gharama nafuu na kuboresha huduma kwa watumiaji. Mwishoni mwa mwaka 2011 kulikuwa na changamoto nyingi katika sekta zinazodhibitiwa na EWURA. Changamoto hizi zilisababishwa na mtikisiko wa kiuchumi duniani na hivyo, soko la dunia lilikabiliwa na kupanda na kushuka kwa bei ya mafuta ghafi.

Mnamo Agosti, EWURA ilifanya mapitio ya kanuni ya bei ya mafuta ya petroli Tanzania Bara, kutokana na kilio cha umma dhidi ya kuongezeka kwa bei ya mafuta ya petroli na kupungua kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani katika soko la fedha za kigeni.

Kanuni hiyo mpya ilipoanza haikupendwa na wafanyabiashara wengi ambao waliamua kuvuruga kwa makusudi usambazaji wa bidhaa za mafuta ya petroli. Mamlaka ilishughulikia changamoto hiyo na kuchukua hatua kali dhidi ya viongozi miongoni mwa wale walioipinga kanuni na kuchochea vurugu zilizotokea. Kwa sasa, hali imedhibitiwa kwa kiwango kikubwa.

Matukio haya yalithibitisha usahihi wa sera za nchi zinazoongoza uagizaji wa pamoja wa bidhaa za mafuta ya petroli. Uagizaji mafuta kwa pamoja ulionekana kama njia bora katika kupunguza hatari zitokanazo na kuvuruga mfumo wa ugavi wa mafuta ya petroli, hasa kama ugavi huo umeungwa mkono na Mkakati wa Hifadhi ya Kitaifa ya Mafuta. Kwa mujibu wa lengo hili, mnamo Septemba 2011, ofisi ya Kuratibu Uagizaji Mafuta ya Petroli (Petroleum Importation Coordinator, PIC ilianzishwa kama chombo cha kisheria chenye kazi ya kuratibu mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja. Mamlaka imekuwa ikifanya kazi na Mratibu wa Uagizaji Mafuta ya Petroli ili kuhakikisha kuwa kipindi cha mpito kutoka kwenye mfumo wa zamani wa uagizaji, ambapo kampuni za mafuta zilikuwa zikiagiza mafuta ya petroli kwa kipekee, kwenda kwenye mfumo mpya wa uagizaji mafuta kwa pamoja unakamilika bila hitilafu yoyote.

Tunaposonga mbele katika suala hili, EWURA ina imani na faida ambazo uchumi utapata kama matokeo ya moja kwa moja kutokana na mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja. Mfumo huu ulianza kwa dhati Januari 2012. Faida hizi ni pamoja na kukomesha uhamishaji wa gharama toka kampuni mama za nchi za nje; kupunguza msongamano wa meli za mafuta bandarini; kupata taarifa za kutosha na kamili juu ya uingizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli; kuhakikisha kuwa bidhaa zote kutoka nje zinaendana na viwango vya ubora vya kitaifa; kuwezesha makampuni (ikiwa ni pamoja na yale ya kati) kushiriki kwa usawa na wale 'wakubwa' katika kuagiza bidhaa bila ya kwenda kwa 'watu wa kati', na hivyo kuendeleza ushindani miongoni mwa wauzaji wa mafuta ya petroli kwa jumla (wholesaler). Tunafahamu kwamba kwa sasa Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) inaandaa Mkakati wa kuwa na Hifadhi ya Kitaifa ya Mafuta.

Kwa upande wa sekta ya umeme, ili kujadili kwa ufanisi matukio ya mwaka 2011, inabidi kuzingatia matatizo ya mgao wa umeme uliosababishwa na masuala ya upungufu wa maji katika mabwawa ya kuzalisha umeme na hali ya ukame ulioukumba nchi nzima. Kwa hali hiyo, EWURA ilitoa leseni kwa mitambo ya dharura iliyonunuliwa na TANESCO kwa msaada wa Serikali. Pia, EWURA ililitathmini ombi la Tanesco la kuongeza gharama za umeme kwa asilimia 155 kwa bidii, uadilifu na uwazi. Uamuzi juu ya suala hilo uliainisha ongezeko la asilimia 40.29, lengo lake ilikuwa kuhakikisha TANESCO itaweza kuendeleza shughuli zake za uzalishaji wa umeme, na wakati huo huo, walaji na uchumi kwa ujumla, wataepukana na ongozeko ambalo ingeweza kuwa kubwa zaidi.

Mwaka 2012, EWURA imedhamiria kudumisha viwango vya kimataifa kuhusiana na uwazi, kuzingatia taaluma, uadilifu, na kufuata sheria za nchi, wakati huo huo kuwashirikisha wadau katika kila hatua itakayoichukua. EWURA itaendelea kuvutia wawekezaji katika sekta za nishati na maji.

Mwisho, napenda kuwashukuru wadau wote kwa ushirikiano wao. Tafadhali ungana nami katika kusoma makala yanayopatikana katika Jarida hili.

Mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja waanza

Na Waandishi wa EWURA

Mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja (Bulk Procurement System—BPS) ulianza rasmi tarehe 4 January 2012, ambapo bei mpya za bidhaa za petroli zinazotokana na kanuni mpya ya kukokotoa bei kwenye mfumo huu zilianza kutumika.
Meli ya kwanza iitwayo MT. Alpine Monique iliyobeba tani 33,000 za dizeli na 7,000 za mafuta ya ndege ilitia nanga kwenye gati la kupakulia mafuta la Kurasini (KOJ) tarehe 6 Januari 2012.

Mfumo huu una maana ya kuwezesha uingizaji nchini Tanzania wa mafuta au bidhaa za mafuta kwa wingi toka chanzo kimoja kwa gharama moja. Hii ni tofauti na mfumo uliopita ambapo kila kampuni ilikuwa inaagiza mafuta toka chanzo chake kwa gharama mbali mbali.

Kwa mfumo huu, zabuni ya kimataifa ya ushindani inabidi itangazwe ili makampuni yanayotaka kutoa huduma hii yashindane, na yeyote atakayeshinda zabuni aweze kuleta bidhaa kwa mujibu wa maombi yao.

Sheria ya kuanzisha BPS
Sheria ya Petroli ya mwaka 2008 inataka uingizaji wa bidhaa za petroli nchini ufanywe kwa ununuzi wenye tija kama ilivyoelezwa na waziri mwenye dhamana ya mambo ya mafuta.

Waziri wa Nishati na Madini alitoa mwongozo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja mwaka 2011 akielekeza kwamba uagizaji wa mafuta yote ya petroli kwa ajili ya soko la Tanzania lazima ufanywe kwa mfumo wa ununuzi wenye tija.Mwongozo huo ambao ulichapishwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 164 la Juni 3, 2011, unaagiza kwamba ununuzi wenye tija utatafsiriwa kama aina ya ununuzi kwa njia ya Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja.

Mara baada ya kutungwa kwa sheria ya Petroli, ukurasa wa 392, mwaka 2008, EWURA ilianza kazi ya kutengeneza mfumo ambao utawezesha mahitaji yote ya bidhaa za petroli kwa ajili ya soko la ndani yatatekelezwa kupitia mfumo wa ununuzi wenye tija.

Utekelezaji wa BPS
Changamoto kubwa kwenye mfumo huu ilikuwa namna gani bora ambayo itawezesha mfumo huu kutekelezwa ili kuleta matokeo yanayotarajiwa bila kuathiri usambazaji wa kawaida wa bidhaa za petroli.

Kwa sababu hiyo, EWURA iliipa kazi kampuni ya kitaalam ya ushauri iitwayo Petroleum Development Corporation (PDC) ya Uingereza kusaidia muundo wa utekelezaji BPS. Mshauri huyo alipendekeza, kati ya mambo mengine, uanzishwaji wa kampuni ya Kuratibu Uagizaji wa Bidhaa za Petroli (Petroleum Importation Coordinator Limited—PIC), ambayo itakuwa na dhamana ya kutaribu uagizaji wa bidhaa za petroli.

Kampuni hii tayari imeanzishwa na kampuni zote za mafuta zenye leseni. Bodi yake inaundwa na wajumbe sita wakiwakilisha kampuni hizo kutegemea uwiano wa mgawanyo wa soko. Kampuni zenye soko la zaidi ya asilimia 10 zinawakilishwa na wajumbe watatu, zenye kati ya asilimia tano na 10 zinawakilishwa na wajumbe wawili, na zenye chini ya asilimia tano zinawakilishwa na mjumbe mmoja katika kuunda bodi ya wakurugenzi ya PIC.

Sambamba na PIC, Waziri wa Nishati na Madini aliunda Kamati ya Ufundi ya Uagizaji wa Mafuta kwa pamoja (Buld Procurement Technical Committee) ambayo pamoja na mambo mengine itafanya yafuatayo:

(a) Kuangalia utekelezaji wa mfumo wa BPS kwa lengo la kuhakikisha unatekelezwa kwa usahihi;

(b) Kuhakikisha kwamba masuala yenye manufaa ya umma yanazingatiwa kwenye mfumo wa BPS ikiwa ni pamoja na usalama wa mfumo wa usambazaji wa mafuta hayo, na mambo yatokanayo na nyakati za dharura katika kusambaza bidhaa za petroli;

(c) Kuchagua mtoa huduma inapotokea kuna uvurugaji wa makusudi wa mfumo wa BPS au ikiwa mratibu wa uingizaji wa bidhaa za mafuta kushindwa kutekeleza wajibu wake

Kutoa zabuni ya kwanza
Zabuni ya kwanza ilifunguliwa 29 Novemba 2011, ambapo wazabuni watano walituma zabuni zao. Hawa walikuwa Vitol geneva SA ya Switzerland; Addax Energy SA; TOTSA (Total International); Augusta Energy SA; na Trafigura PTE Limited. Mshindi wa zabuni alikuwa Augusta Energy SA. Muda wa kutoa kuduma kwa zabuni ya kwanza ni miezi ya januari na Februari 2012.

Faida za BPS
Kati ya mambo mengine, zifuatazo ni faida za mfumo huu wa BPS;

(a) Kuepuka msongamano wa meli bandarini kwa kuwa meli zitakuwa zinawasili kwa kufuata ratiba, hivyo kupunguza au kuondoa kabisa gharama za tozo zitokanazo na meli kukaa muda mrefu bandarini (demurrage charges);

(b) Upatikanaji wa takwimu sahihi za bidhaa za petroli na kurahisisha ukusanyaji wa mapato, na;

(c) Mizania ya kiuchumi inayoleta malipo ya kiwango cha chini na hivyo kumnufaisha mtumiaji.

Meli ya MT. ALPINE MONIQUE ikipakua shehena ya kwanza ya mafuta katika mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja kwenye eneo la kupakulia mafuta, Kurasini, Januari 2012.

Mafanikio ya kihistoria katika kuidhinisha bei

Utekelezaji wa bei hizi mpya zilizopatikana kwa kutumia kanuni ya ugezaji umepokelewa vyema na wadau katika mamlaka nyingi

Na Titus Safari

Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeweka rekodi ya kihistoria kwa kuidhinisha ongezeko la bei za huduma za maji kwa Mamlaka 89 za Maji na Usafi wa Mazingira zilizo katika ngazi ya Miji mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa (DWSSAs).

Hii ni mara ya kwanza kwa EWURA tangu kuanzishwa kwake mwaka 2006 kuidhinisha mabadiliko ya bei kwa idadi kubwa kama hii ya mamlaka za maji kwa mara moja. Ongezeko hilo la bei liliidhinishwa kupitia Agizo la EWURA Na. 11-014 na lilianza rasmi tarehe 1 Juni, 2011.

Mabadiliko haya ya bei yanategemea kuziwezesha DWSSAs kufikia bei zinazorejesha gharama za uendeshaji kwa upande mmoja na kutoa huduma bora na za uhakika kwa wateja wao kwa upande mwingine.

Mabadiliko haya ni sambamba na Sera ya Maji ya mwaka 2002 (NAWAPO 2002) ambayo Serikali imeweka wazi dhamira yake ya kuona kuwa kila Mamlaka ya Maji inarejesha gharama zote za kutoa huduma kwa wateja wake (full cost recovery) kwa muda wa kati hadi mrefu. Kurejesha gharama zote za uendeshaji inamaanisha kurejesha gharama za uendeshaji na matengenezo, uchakavu na uwekezaji.

Hatua hii ya EWURA imezingatia pia matokeo ya zoezi la tathmini ya uwezo wa Mamlaka za Maji za Miji ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Maji ya kitaifa (DWSSAs) lililofanywa na EWURA kwa kushirikiana na Wizara ya Maji. Zoezi hilo lilibaini kuwa DWSSAs nyingi zina matatizo yanayofanana.

Baadhi ya matatizo hayo ni pamoja na uchakavu wa miundombinu, uhaba wa fedha kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa huduma, uwezo mdogo watumishi katika usimamizi, bei ndogo ya huduma, kukosekana kwa taarifa na takwimu na kutosimamia na kutunza vyema vyanzo vya maji.

Kutokana na changamoto hizo zinazokabili DWSSAs, EWURA iliandaa Mwongozo wa Kupanga Bei kwa Mamlaka za Maji za Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Maji ya Kitaifa wa mwaka 2011. Mwongozo huo umelenga kuweka utaratibu wa kurekebisha tofauti zilizopo kati ya DWSSAs na pia kuziwezesha kufikia hatua ya kurejesha gharama zote zote za kutoa huduma.

Mwongozo huo umezingatia taratibu za kupanga bei na tozo chini ya Sheria ya EWURA Sura 414 na pia malengo yaliyo katika Sera ya Maji ya mwaka 2002 ya kuwa na Mamlaka za Maji zilizo endelevu. Kwa hatua hii EWURA imetoa mchango mzuri katika kuendeleza Sekta ya Maji nchini Tanzania kwa kutengeneza moja ya nyenzo muhimu katika utekelezaji wa Sera ya Maji.

Mwongozo huo wa mwaka 2011 unaonesha kuwa marekebisho ya bei kwa DWSSAs yatafanywa kwa kwa kutumia Kanuni ya Ugezaji (Indexation Formula). Kanuni ya ugezaji hukokotoa bei kwa kulinganisha bei na tozo za DWSSAs na zile za Mamlaka za Maji zinazotoa huduma katika Miji Mikuu ya Mikoa (RWUs) kwa kila kundi la wateja.

Bei na tozo ambazo ziko juu ya zile zinazotozwa na RWUs hazitabadilishwa lakini DWSSAs zilizoko katika kundi hili ziko huru kuomba mabadiliko ya bei kwa kuzingitia Mwongozo wa Kurekebisha Bei uliotolewa mwaka 2009. Bei za maji kwenye magati (vioski) zitakuwa asilimia 70 ya bei za wateja wa majumbani zikiwa zimekadiriwa kwa shilingi 5 ya karibu. Hata hivyo, kiwango cha juu cha bei kwenye magati kitakuwa shilingi 20 kwa ndoo ya lita 20. Kiwango hicho cha juu kinaweza kutathminiwa tena pale itakapobidi.

Katika kuandaa Kanuni hii ya Ugezaji ambayo imetumika kukokotoa bei mpya zilizomo ndani ya Agizo Na. 11-014, EWURA ilikusanya na kuzingatia maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na DWSSAs, Baraza la Watumiaji wa Huduma zinazothidhibitiwa na EWURA (EWURA CCC) na Baraza la Ushauri la Serikali (GCC).

Hii ni kwa kuzingatia kifungu cha 19(2)(h) cha Sheria ya EWURA Sura 414. Pamoja na kuidhinisha ongezeko la bei, katika Agizo hilo EWURA imezitaka DWSSAs kuwasilisha taarifa kama zitakavyotakiwa mara kwa mara. DWSSAs zitakazoshindwa kutimiza sharti hilo zinaweza kuondolewa katika utaratibu wa ugezaji wa bei. Kuondolewa kwenye utaratibu wa ugezaji kunaweza pia kutokana na kutotekeleza maagizo yanayoweza kutolewa na EWURA wakati wa kusimamia utendaji wa mamlaka husika.

Kwa ujumla, utekelezaji wa bei hizi mpya zilizopatikana kwa kutumia kanuni ya ugezaji umepokelewa vyema na wadau katika mamlaka nyingi. Hata hivyo, yapo maeneo machache ambapo wadau wamesita kuzikubali bei mpya hasa kutokana na kutoelewa mamlaka na wajibu wa EWURA na mchakato mzima wa kupanga bei. Uma unahitaji pia kuelewa utaratibu wa kufuata katika kupinga maamuzi/maagizo yaliyotolewa na EWURA. EWURA itaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu maswala haya.

Mamlaka za miji midogo sasa zitakuwa na uwezo wa kuifanyia matengenezo miundombinu ya maji kama tanki hili la Tukuyu, ambalo linatumika kwa asilimia 25 tu ya uwezo wake kwa sababu linavuja.

EWURA yasimamisha ujenzi wa vituo 25 kwa kukiuka masharti

Nia ya ukaguzi huo ilikuwa kubaini vituo vinavyojengwa kinyume cha sheria na kuvichukulia hatua kwa mujibu wa Sheria ya bidhaa za Petroli, Sura ya 392, na kuhakikisha kuwa bidhaa za petroli zinazouzwa sokoni zinakidhi mahitaji ya viwango vya Tanzania.

Na Wilfred Mwakalosi

Ukaguzi wa kushtukiza uliofanywa na Mkaguzi Mkuu wa Petroli kati ya mwezi Machi na Aprili 2011 kwenye baadhi ya mikoa umebaini kuwa vituo 25 vya mafuta vilivyokuwa vikijengwa, vilikuwa vikijengwa kwa kukiuka sheria za ujenzi.

Ukaguzi huo ulifanyika kwenye mikoa ya Pwani, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora na Shinyanga. Mkaguzi mkuu wa petroli wa EWURA Bw. Julius Gashaza amesema nia ya ukaguzi huo ilikuwa kubaini vituo vinavyojengwa kinyume cha sheria na kuvichukulia hatua kwa mujibu wa Sheria ya bidhaa za Petroli, Sura ya 392.

Alisema vituo hivyo vilibainika kukiuka mwongozo wa sheria ya bidhaa za petroli. Hivi karibuni, EWURA iliidhinisha ujenzi wa vituo vitano vya mafuta: Dar Express Petrol Station cha Moshi; Gapco (T) Ltd cha Tunduma, Mbeya; MGS International cha Mkuranga, Pwani, TOTAL (T) Ltd cha Mlimani City, Dar es Salaam; na Big Bon cha Sinza, Dar es Salaam.

Licha ya ukaguzi wa ujenzi wa vituo, EWURA imekuwa ikiendesha ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha kuwa bidhaa za petroli zinazouzwa sokoni zinakidhi mahitaji ya viwango vya Tanzania.

Zaidi ya hayo, vituo viwili vya mafuta vilifungwa kwa kushindwa kufuata kanuni za kiusalama za Afya, Usalama na Mazingira. Vituo hivyo ni Onakiro Olomi Sakina Petrol Station, Arusha, na ghala dogo la kampuni ya mafuta ya Mount Meru huko Tabata, Dar Es salaam.

Mwongozo wa EWURA unaelezea, pamoja na mambo mengine, vigezo vinavyotakiwa kuzingatiwa hasa kiufundi, miundombinu, afya, usalama na mazingira katika ujenzi na uendeshaji wa biashara ya rejareja kwa bidhaa za petroli nchini Tanzania. Mwongozo huu pia unasaidia wanaotaka kuwekeza kwenye biashara hii.

Mwongozo unaelekeza kuwa eneo lililochaguliwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mafuta lichaguliwe kwa vigezo kuwa litapunguza kwa kiwango kikubwa hatari kwa maisha na mali zilizo jirani. Pia lazima izingatiwe hatari iliyopo juu ya kituo cha mafuta endapo mali za jirani zitapata ajali.

Mombaji wa ujenzi atachukua tahadhari pia ya ujirani wa njia za umma, umuhimu wa kuepuka kujenga jirani na miundombinu ya maji; na tahadhari dhidi ya hatari ya maeneo ya jirani; aina na wingi wa bidhaa zitakazohifadhiwa; na umuhimu wa kujihadhari kujenga karibu na makazi yenye watu wengi na uwezekano wa kudhuru huduma mpya kwenye maeneo kama hayo.

Kiwango cha chini kabisa kwa kituo cha biashara ya reja reja inabidi kuzingatia kwamba matanki ya hifadhi ya mafuta na pampu pamoja na mabomba yajengwe kwa namna ya kuzuia uvujaji wowote wa mafuta; eneo la mashine za kusukuma mafuta liwe limejengwa kwa sakafu nzuri na lenye mifereji iliounganishwa kwenye mtambo wa kuchujia ama maji au vilainishi.

Inabidi pia tanki la kuhifadhia mafuta liwekewe bomba la kutolea hewa lenye kipimo cha angalau mita 3.5 urefu; na kila eneo linalozunguka pampu liwekewe vizuizi vya urefu wa mita moja toka chini kuzuia zisigongwe; na angalau eneo la mashine za kusukumia mafuta ziwe zimefunikwa kwa paa lenye kuzingatia ujenzi bora wa maeneo ya mafuta.

Baadhi ya maelezo kuhusu namna ya kujenga na kuweka matenki na mabomba ya ardhini, mitambo ya umeme wa dharura, mitambo ya kutenganisha vilainishi, namna ya kutengeneza eneo la pampu, mabomba ya kutolea hewa nk. yanaweza kupatikana toka viwango vya ubora TZS 1115: 2009: Ubora wa vituo vya kuuzia bidhaa za petroli na TZS 1079: 2009: Ubora wa ujenzi wa mghala ya kutunzia mafuta ardhini, pampu za mafuta mabomba yanayounganisha matanki na pampu.

Ushiriki wa EWURA kwenye maonesho waimarisha kampeni ya elimu kwa umma

Na Wilfred Mwakalosi

Mkaguzi Mkuu wa Bidhaa za Petroli wa EWURA, Mhandisi Julius Gashaza (kushoto) na Meneja Biashara—Umeme Norbert Kahyoza (kulia), wakimhudumia mteja aliyetembelea banda la EWURA wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya Kibiashara ya Dar es Salaam Julai 2011.

Ushiriki wa hivi karibuni wa EWURA kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam, Maonesho ya Wakulima yaliyofanyika mkoani Dodoma (Nane Nane), na Maonesho ya shughuli za Taasisi zilizo kwenye Wizara ya Nishati na Madini bungeni Dodoma kumetoa nafasi nzuri kwa Mamlaka ya EWURA kuimarisha kampeni yake ya Elimu kwa Umma, jambo ambalo ni muhimu katika kufanikisha majukumu yake.

Maonesho ya 36 ya Saba Saba, yalianza Juni 28, 2011 na kumalizika Julai 8, 2011. EWURA ilishiriki kwa mara ya kwanza kwenye maonesho hayo, ikiwa imekosa kushiriki mara nne kwa misimu iliyotangulia tangu ianze kufanya kazi mwaka 2006.

Kwa mamlaka ya udhibiti ambayo ingependa shughuli zake zifahamike kwa umma, huu ulikuwa wakati muafaka ambao isingewezekana kuukosa, alisema Mkuu wa Mawasiliano na Uhusiano wa Umma Bw. Titus Kaguo.

Kwenye maonesho yote ya Saba Saba na Nane Nane, banda la maonesho la EWURA lilikuwa na maofisa waandamizi kutoka idara za sekta zote nne zinazodhibitiwa; Umeme, Bidhaa za Petroli, Gesi Asilia na Maji.

Wageni waliotembelea banda la EWURA walisema walifurahi kupata nafasi ya kujifunza namna Mamlaka inavyoendesha shughuli zake, lakini wakaomba elimu zaidi itolewe kwa umma.

Katika maonesho hayo, mara nyingi wageni hao walikuwa na shauku ya kufahamu sababu za kubadilika kwa bei ya bidhaa za petroli, namna gani uchakachuaji wa mafuta unavyodhibitiwa, marekebisho ya bei ya mafuta ya taa katika kupambana na uchakachuaji, na Gesi Asilia.

Wengine walitoa wito kuongezwa kwa elimu kwa umma, wakisema ingawa Mamlaka ya EWURA inaweza kuwa inafanya kazi nzuri, bado watu wengi hawana uelewa juu ya mambo muhimu kuhusu shughuli zake.

Bw. Praygod Makundi, mmoja wa watu waliotembelea banda la EWURA wakati wa Saba Saba alitoa maoni yake kwenye kitabu cha wageni: “Wakati mnafanya kazi nzuri, umma haufahamu kazi zenu. Ni muhimu mkaongeza elimu kwa umma kuhusu EWURA.”

Huko Dodoma, maonesho ya wiki nzima ya Nane Nane pia yalitoa mwanya kwa EWURA kuktana na kuongea na watu wa aina mbali mbali kutoka mikoa ya katikati mwa Nchi. Wengi wa waliotembelea banda la EWURA walikuwa wakiulizia sana juu ya kazi za Mamlaka na namna ambavyo zinahusika na maisha yao ya kila siku.

Mwishoni mwa mwezi Agosti, Mamlaka ilipata nafasi nyingine ya kuonesha shughuli zake iliposhiriki kwenye maonesho kwa wabunge, kwenye viwanja vya Bunge mjini Dodoma. Kwenye maonesho hayo, ulikuwepo pia mtambo maalum kwa ajili ya kupimia mafuta yaliyochakachuliwa nay ale ambayo hayajalipiwa ushuru.

Wakurugenzi wa Bodi watembelea mamlaka za maji Kaskazini

Na Wilfred Mwakalosi

Wakurugenzi wa Bodi ya EWURA, Bi. Juliana Mwalongo na Bw. Nicholaus Mbwanji mwezi Julai mwaka huu walitembelea Mamlaka za ya Maji safi na Maji taka kwenye mikoa ya kanda ya kaskazini ya Tanga, Arusha na Moshi, ambako walipata nafasi ya kujifunza shughuli za uendeshaji wa sekta hiyo inayodhibitiwa na EWURA.

Wakati wa ziara yao, wakurugenzi wa Bodi walipendekeza mamlaka hizo za maji safi na maji taka kwenye mikoa hiyo mitatu kutafuta mikopo toka taasisi za fedha ili kusaidia kutimiza wajibu wao wa kiuwekezaji, badala ya kutegemea misaada toka serikalini, ambayo mara nyingi huwa inakosekana.

Wamesema licha ya mafanikio yaliyopatikana, mamlaka hizo inabidi kujipanga vizuri zaidi ili kuongeza ufanisi wa huduma kwa wateja kwa sasa na kwa siku zijazo.

Ziara hiyo ya kujifunza ilihusisha kutembelea vyanzo vya maji, miundombinu ya kusambazia maji safi na maji taka, na ofisi. Wakurugenzi pia walijadiliana na wakurugenzi wenzao na menejimenti za mamlaka hizo juu ya mambo mambo muhimu ya kiuendeshaji mamlaka hizo.

Kwenye Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mjini Tanga (Tanga Urban Water and Sanitation Authority—Tanga UWASA), ujumbe wa EWURA ulielezwa kwa kifupi juu ya shughuli za Mamlaka na Mkurugenzi mtendaji Mhandisi Joshua Mgeyekwa kwenye mkutano ulioongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi wa Tanga UWASA, Mhandisi Raymond Mhando.

Ujumbe huo pia ulitembelea matangi ya kuhifadhia maji ya Kange na Nguvumali bwawa la Mabayani, Kituo cha kusukuma maji cha Mabayani, Mtambo wa kusafisha maji taka wa Mowe, Kituo cha kusukuma maji taka na eneo la kumwaga maji taka baharini.

Wakurugenzi wa Bodi wa EWURA waliridhishwa na taarifa kuwa maji mkoani humo yanapatikana kwa saa 24, kwa siku, na kwamba yanakidhi viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS), wakati asilimia 99 ya wakazi wanaohudumiwa na mamlaka hiyo wanapata huduma.

Walipokuwa Mabayani, ujumbe ulishuhudia namna vyanzo vya maji vinavyotunzwa, ikiwa ni pamoja na kupandwa kwa miti stahili na usimamizi thabiti wa vyanzo vya maji kwa kutumia kamati za pamoja baina ya wanavijiji na Mamlaka.

Mhandisi Mgeyekwa aliuambia ujumbe kwamba mamlaka yake ina ubora wa kukusanya mapato unaofikia asilimia 98, na kwamba Tanga UWASA ina cheti cha ubora wa kimataifa cha ISO 9001, ikiwa na maana kwamba taratibu zote za kiuendeshaji zinawekwa kwenye maandishi, zinafuatiliwa na zinakaguliwa na kuhakikiwa na wakaguzi wa mahesabu wa ndani na nje.

Hata hivyo, licha ya mafanikio yaliyopatikana, Wakurugenzi wa EWURA walipendekeza kwamba kwa kuwa Tanga UWASA imefikia asilimia 100 katika usambazaji wa maji, katika mkakati wa kibiashara inafaa ianze kupanua wigo wa wateja wake na kuongeza tafiti ili kuongeza ufanisi wa shughuli zake.

Wakurugenzi wa Bodi ya EWURA, Bi. Juliana Mwalongo na Bw. Nicholaus Mbwanji wakimsikiliza kwa makini ofisa wa mamlaka ya Maji safi na Maji Taka Tanga, akiwaelezea juu ya mtambo wa kusafisha maji wa Mowe walipotembelea mamlaka hiyo mwezi Juni, 2011.

Mjini Moshi, ujumbe ulitembelea Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Mjini humo, (Moshi Urban Water and Sanitation Authority –MUWSA), ambapo ukiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka Bw. Antony Kasonta, na Mkurugenzi wa Bodi ya MUWSA, Bw. Paul Chikira, ulitembelea vyanzo vya maji vya Nsere na Shiri, Tangi la kuhifadhia maji safi la Kilimanjaro, Mtambo wa kusafishia maji taka wa Mabogini na eneo la kuuzia maji lenye dira ya maji za malipo kabla huko Kiboroloni.

Ujumbe wa EWURA uliipongeza MUWSA kwa utendaji mzuri, ambapo licha ya maji yake kukidhi viwango vya TBS, inawafikia kwa asilimia 98 wateja wake, ambamo pia wamewekwa dira wote, na ankara za maji zinapelekwa kwa mkono.

Ilionekana pia kwamba utunzaji wa vyanzo vya maji ni wa hali ya juu, ambapo miti husika imepandwa na uzio umejengwa kuzunguka eneo la chanzo cha maji. Mamlaka pia imeweza kukusanya mapato kwa aslimia 96, wakati huduma za maji taka zinapatikana kwa asilimia 44, kikiwa ni kiwango cha juu kabisa kufikiwa na mamlaka nchini. Maji taka ya MUWSA yanakidhi viwango vya ubora vya TBS kiasi kwamba yanatumika kwa kilimo cha mpunga.

Mkoani Arusha, wakiongozwa na kaimu Mkurugenzi mtendaji, Mhandisi Ruth Koya, Wakurugenzi wa bodi ya EWURA walitembelea eneo la mchepuo wa maji kwenye mto Nduruma na mtambo wake wa kushafisha maji, Chemchem ya Olesha Masama, visima vya Kiranyi na Sekei, mtambo wa kusafisha maji, chumba cha mitambo ya kuongozea na matangi ya kuhifadhia maji ya Sekei, na mitambo ya kusafishia maji ya Lemara.

Kama ilivyokuwa kwa mamlaka nyingine mbili za Tanga na Moshi, huduma za maji AUWASA zimeenea kwa asilimia 98.5 ya watu walio kwenye eneo linalohudumiwa, na asilimia 100 ya wateja wamefungiwa dira za maji, Ankara zinapelekwa kwa mkono huku vyanzo vya maji vikitunzwa kwa kupanda miti na kuzungungushia uzio. Ukusanyaji wa mapato ni wa asilimia 96.5.

Ili kujihakikishia upatikanaji wa maji toka kwenye vyanzo vyake ambavyo vingi viko wilaya ya Arumeru, ushauri ulitolewa kwamba AUSA iangalie uwezekano wa kupanua eneo la kutoa huduma ili kuhudumia maeneo ambayo kuna vyanzo vya maji yake.



Maporomoko ya maji kwenye mto Nduruma, moja ya vyanzo muhimu vinavyotoa huduma ya maji kwa wakazi wa Arusha.

EWURA: “Kazi yetu sasa inatambulika”

Wafanyakazi wa EWURA wakiwa katika picha ya pamoja Septemba mosi, 2011, walipoadhimisha miaka mitano tangu kuanzishwa kwa EWURA, Septemba 2006. Umma sasa unatambua kazi na wajibu wa mamlaka

Na Mwandishi wa EWURA

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati (EWURA) imesisitiza kwamba mamlaka za udhibiti nchini zimeisaidia serikali kuongeza mapato yake na kuimarisha bei za bidhaa kuliko kuwa mzigo kwa walipa kodi.

Mkuu wa Mawasiliano na Uhusiano wa Umma wa EWURA, Bw. Titus Kaguo alisema hayo hivi karibuni ikiwa ni kujibu hoja zilizotolewa na wakosoaji, kwamba mamlaka nyingi za usimamizi na udhibiti sasa ni mzigo.

“Kwa mfano, tangu EWURA ianzishe uwekaji vinasaba kubaini uchakachuaji na uuzaji nchini wa mafuta yasiyolipiwa kodi, kiwango cha mafuta yanayoingizwa nchini na cha kodi zinazolipwa serikalini kimeongezeka sana,” alisema Bw. Kaguo.

Uwekaji vinasaba umeisadia Mamlaka kubaini uchakachuaji na wizi wa mafuta yaendayo nje ya nchi, ambapo kwa upande mwingine, imeisaidia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuongeza makusanyo ya kodi kufikia bilioni 170.9/- kwa mwaka, Bw. Kaguo alisema.

Akifafanua umuhimu wa EWURA, Bw. Kaguo alisisitiza kuwa kabla Mdhibiti kuanza matumizi ya vinasaba kwenye mafuta, petroli iliyokuwa ikiingizwa nchini ilikuwa wastani wa lita milioni 34.6 kwa mwezi, lakini sasa imeongezeka kwa lita milioni 10 milioni kufikia wastani wa lita milioni 44.01 kwa mwezi.

“Ongezeko la asilimia 27 kwa mwezi limesababisha kuongezeka kwa mapato kufikia bilioni 60.9/- kwa mwaka,” alisema.

Kwa dizeli, kabla ya kuweka vinasaba lita milioni 69.2 zilikuwa inaingizwa nchini lakini zikaongezeka hadi kufikia lita milioni 87.06, ikiwa ni ongezeko la asilimia 26. Haii inaleta mapato ya ya wastani wa bilioni 110.061/- katika kodi.

Kinachoshangaza ni kuwa, wakati waagizaji mafuta wangeingiza lita milioni 30.025 za mafuta ya taa kwa mwezi kabla ya uwekaji vinasaba, sasa wanaingiza lita milioni 19.005 kwa mwezi, ikiwa ni punguzo la lita milioni 11.020 (asilimia 37).

“Mwenendo huu unathibitisha kwamba mafuta ya taa yalikuwa yakitumika kuchakachua, na kuikosesha serikali mapato,” Bw. Kaguo alifafanua.

Uchambuzi wa biashara ya uagizaji mafuta unaonyesha kuwa kuna aina mbali mbali nane za tozo zinazolipwa kwenye taasisi za umma, wakati aina nyingine 13 ni tozo za makampuni ya uagizaji mafuta, kodi na gharama za uagizaji.

Taasisi za serikali zinazokusanya tozo kwenye mafuta yanayoagizwa nje ni pamoja na EWURA, TRA, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Bw. Kaguo alisema uchambuzi zaidi wa EWURA umehitimisha kwamba tozo za mafuta zinazotozwa na taasisi za serikali ni asilimia 2.6 tu ya gharama husika na kwamba gharama zote za ndani ya nchi, ikiwa ni pamoja na za makampuni ya mafuta ni asilimia 4.26 tu ya bei ya reja reja.

“Katika hali hii, kama ingebidi tufute asilimia 2.6 ya tozo hizo

tungekuwa tunaondoa 47/- tu kwa lita, je, tunataka tuondoe Mamlaka za Udhibiti kwa kiasi hiki kidogo cha tozo? " aliuliza. Kwa mujibu wa Bw. Kaguo, baadhi ya nchi za Kiafrika zimekuja Tanzania kujifunza namna ambavyo EWURA imeweza kufanikiwa kudhibiti sekta nne mbali mbali kwa pamoja. Alizitaja nchi hizo kuwa ni Lesotho, Uganda, Msumbiji na Kenya.

Maonesho ya namna ya upimaji wa sampuli za mafuta: Mradi wa kuweka vinasaba kwenye mafuta ili kudhibiti uchakachuaji na wizi wa mafuta yaendayo nje ya nchi umewezesha pia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuongeza ukusanyaji wa mapato ya mafuta kufikia Tsh 170 bilioni kwa mwaka. Kabla ya hapo, petroli ilikuwa ikiingizwa lita milioni 34.6 kwa mwezi, lakini sasa imeongezeka kwa lita milioni 10 hadi kufikia lita 44.0 kwa mwezi.

Rais apongeza uimara wa EWURA

Aipongeza EWURA kwa kuwa imara na thabiti katika sekta inazodhibiti, na kuitaka kuendelea na moyo huohuo na kuwaadhibu wote wanaokiuka kufuata maelekezo yake.

Na Wilfred Mwakalosi

Rais Jakaya Kikwete akiwa mwenye furaha alipokutana na Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Bw Haruna Masebu kwenye viwanja vya Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa Dar es Salaam, wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya Uhuru mwezi Desemba 2011.

Rais Jakaya Kikwete amewataka wafanyabiashara ya mafuta kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) katika utendaji wa majukumu yake.

Akihutubia Taifa katika kuukaribisha mwaka mpya 2012, Rais alisema mwenendo wa wafanyabiashara wa mafuta kutokukubali maamuzi ya EWURA hususan pale bei ya mafuta inaposhuka imekuwa ni tatizo.

“Wafanyabiashara wa mafuta hawapo tayari kupunguza bei ya mafuta hasa pale bei zinaposhuka, hawapo tayari kuona watumiaji wakipata nafuu hata kidogo,” Rais alisema.

Rais alisema pia wafanyabiashara aidha huendelea kuuza mafuta katika bei ya juu au kutengeneza hali ya upungufu wa bidhaa hiyo ili bei ibaki kuwa juu.
“Hata hivyo, mara tu EWURA inapotangaza kupanda kwa bei za mafuta, mambo haya ya mafuta kuwa hadimu hatuyaoni,” alisema Mheshimiwa Rais.

Rais alisisitiza pia kugoma kushusha bei za mafuta nchini wakati bei katika soko la dunia imeshuka ni kwenda kinyume na haki za binadamu.

Rais aliipongeza EWURA kwa kuwa imara na thabiti katika mambo inayosimamia, na kuitaka kuendelea na moyo huohuo wa kuwaadhibu wote wanaokiuka kufuata maelekezo yake. Rais Kikwete pia alisema kwamba nchi inapoelekea katika mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja kutapunguza gharama za uagizaji na hivyo kufanya bei ya bidhaa iyo kushuka kufikia hali halisi ya mtumiaji.

“Mfumo huu wa uagizaji mafuta kwa pamoja utaanza mwezi huu (Januari). Naamini utasaidia, labda kama utakwamishwa. Tusubiri tuone namna gani utakavyosimamiwa” alisema. Rais aliiagiza wizara na mamlaka zinazohusika kuhakikisha mfumo wa uagizaji mafuta kwa pamoja unafanikiwa kama inavyotarajiwa.

Kwa upande mwingine, vituo vitano vya kuuza mafuta vilifungwa na leseni zake kusitishwa kwa muda kufuatia kukiuka agizo la bei elekezi mafuta iliolotolewa na EWURA katikati ya mwezi Disemba. Vituo vilivyofungwa ni GBP Petrol Station (Sinza), Camel Oil (Tabata), GAPCO (Mbagala Rangi Tatu), na Camel Petrol Station (Ausha) vinavyomilikiwa na Madar Enterprises). Hata hivyo vituo hivyo vilifunguliwa baadaye.

Ofisa Mkuu wa Mawasiliano na uhusiano, Bw. Titus Kaguo alisema wafanyabiashara walipopewa agizo la kufuata masharti, GBP alikataa kupokea agizo hilo. “GBP Petrol station alikataa kupokea agizo la kufuata masharti yetu hivyo moja kwa moja kituo kikafungwa na leseni yake kufutwa,” Kaguo alisema.

Aliongeza pia Camel Oil (Arusha) itafungwa na kupewa siku saba kueleza kwanini leseni yake isisitishwe. Kituo hicho hakikuuza mafuta licha ya kuwa na akiba ya kutosha.

“Tumepeleka swala hili kwa Mwendesha mashtaka wa serikali (DPP) illi kuwashitaki waliogoma kuuza mafuta kwa kosa la uhujumu uchumi”. Alisema Kaguo.

Katikati ya mwezi Disemba 2011, Dar es salaam ilikumbwa na uhaba wa petroli na kusababisha misururu mirefu ya magari ikiwa ni siku moja tangu EWURA itangaze kushuka kwa bei ya petroli.

Aidha, Rais alisema TANESCO imezidiwa na mzigo wa gharama za uendeshaji hivyo gharama ya bei ya umeme kupanda haiepukiki. Hata hivyo mheshimiwa rais alisema upatikanaji wa gesi asilia na matumizi yake katika uzalishaji wa umeme utapunguza sana gharama za umeme.

Kamati ya Bunge yapongeza punguzo la tozo za mafuta...

Lakini yatahadharisha ongezeko la bei ya mafuta soko la dunia

Hata hivyo, kamati ilisisitiza kwa serikali kuongeza elimu kwa umma juu ya ukweli kuhusu bei ya mafuta kwenye soko la dunia, ambalo serikali haina uwezo wa kulidhibiti.

Na Wilfred Mwakalosi

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi imeipongeza serikali kwa hatua ilizochukua kupunguza bei za mafuta nchini katika jitihada za kupunguza mzigo wa kiuchumi kwa wananchi wake.

Akiwasilisha bungeni maelezo ya kamati yake kuhusu utendaji wa Wizara ya Fedha kwa mwaka 2011/2012, mwenyekiti wa kamati hiyo Mh. Dk. Abdallah Kigoda alisema hatua ya serikali ya kuangalia upya na kudhibiti bei za mafuta, na zile za bidhaa zingine mbali mbali, kama ilivyopendekezwa na na kamati hiyo mwaka 2010 ilikuwa ya kutia moyo.

Kupitia chombo chake cha udhibiti—Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), serikali mnamo mwezi Julai 2011 iliamua kutazama upya tozo mbali mbali za bidhaa za petroli na ikaongeza tozo kwenye mafuta ya taa na kupunguza kodi ya mafuta ya dizeli ili kupunguza uchakachuaji.

“Kamati inaipongeza serikali kwa hatua zake hizi za kupunguza bei ya mafuta, hasa kwa dizeli na petroli, kwa kupunguza tozo zilizoko kwenye mafuta haya yanapoingizwa nchini,” aliliambia Bunge hivi karibuni.

Hata hivyo, kamati ilisisitiza kwa serikali kuongeza elimu kwa umma juu ya ukweli kuhusu bei ya mafuta kwenye soko la dunia, ambalo serikali haina uwezo wa kulidhibiti. Alisema hata kama serikali inapunguza tozo za mafuta wakati bei ya soko la dunia inazidi kupanda, hakutakuwa na unafuu unaokusudiwa kwa watumiaji wa huduma hizo.

“Unafuu wa kiuchumi utapatikana pale tu ambapo bei za soko la dunia zipungua,” alisema, na kuongeza kuwa kwa nchi haina uwezo wa kudhibiti bei hizo katika soko la dunia, nchi hujikuta ikipata matatizo ya kiuchumi. Mh. Dk. Kigoda alisema kamati yake inaona kwamba faida kubwa za kiuchumi zitapatikana pale tu ambapo mpango wa uagizaji mafuta kwa pamoja utakapoanza.

Tayari EWURA imeanza mchakato wa kukusanya maoni toka kwa wadau, juu ya namna ambavyo kanuni ya kukokotoa bei ya mafuta itaendana na mfumo mpya wa kuagiza mafuta kwa pamoja.

Waziri wa Nishati na Madini, Mh. William Ngeleja (Kulia) akikaribishwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA, Bw. Simon Sayore kwenye moja ya mikutano ya mwaka 2011 kuhusu sekta ndogo ya petroli. Kamati ya Bunge ya Uchumi na Fedha imeridhishwa na upunguzaji tozo kama sehemu ya juhudi za kupunguza bei ya mafuta.

Uchakachuaji, uingizaji wa mafuta ya taa nchini wapungua

Mkaguzi wa Petroli, Mhandisi Nathaniel Edward (kushoto) akionesha namna ya kupima sampuli za mafuta ili kubaini uchakachuaji. Wanaoangalia ni Mwenyekiti wa Baraza la watumiaji wa huduma za nishati na maji, Prof. Jamidu Katima, (wa pili kulia), na Katibu wa Baraza hilo, Mhandisi Goodluck Mmari (kulia)., na Mkaguzi MKuu wa Petroli wa EWURA, Mhandisi Julius Gashaza (wa tatu Kulia).

Na Wilfred Mwakalosi

Kumekuwa na matukio machache ya uchakachuaji wa mafuta ya bidhaa zitokanazo na petroli kuliko hali ilivyokuwa kabla ya September 2010, wakati ambapo EWURA ilianza kuweka vinasaba kwenye bidhaa za petroli Tanzania Bara.

Pamoja na ukaguzi wa uchakachuaji, EWURA pia hufanya ukaguzi wa mafuta yaendayo nje ya nchi, ambayo kwa kawaida kuwa hayalipiwi kodi lakini yanaweza kuingizwa kwenye soko la ndani na wafanya biashara wasio waaminifu. Katika ukaguzi wa eneo hili, matokeo mazuri yameweza kuonekana.

Kumekuwa na ongezeko la utiifu wa sheria na kanuni kwa makampuni ya usambazaji mafuta kwa kuuza bidhaa zenye ubora unaotakiwa. Kwa ujumla, uchakachuaji umepungua toka asilimia 78 Mei 2007, hadi kufikia asilimia 10 tu mwezi Juni 2011, hasa kutokana na ukaguzi wa kushtukiza, kuanzishwa kwa teknolojia ya uwekaji vinasaba, ,na serikali kurejesha tozo katika mafuta ya taa.

Ukaguzi ulifanyika mara kadhaa, ambapo kati ya Julai 2010 na Jui 2011, jumla ya sampuli 214 zilichukuliwa toka makampuni ya jumla na reja reja kwa ajili ya kupima ubora. Kati ya sampuli zilizopimwa, jumla ya sampuli 21 zilibainika kuwa na matatizo. Hatua kali zilichukuliwa dhidi ya wahusika waliokutwa na mafuta yasiyokidhi viwango.

Kati ya Julai 2010 na Juni 2011, vituo 380 vya petroli vilichukuliwa sampuli Tanzania Bara ambapo vituo 83 kati ya hivyo vilikutwa na mafuta yenye matatizo, sawa na asilimia 22 ya sampuli zote zilizopimwa. Vituo vya mafuta vilivyokutwa na mafuta ya kwenda nje ya nchi yaliyokuwa hayajalipiwa kodi vilikabidhiwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kulipia kodi stahiki. TRA inasema sh. Milioni 300 zililipwa.

Vivyo hivyo, magari 161 ya kusafirisha shehena za mafuta kwenda nje ya nchi yalichukuliwa sampuli, ambapo magari yote yalikutwa na mafuta yenye ubora unaotakiwa. Zaidi ya hayo, magari 24 kwa ajili ya shehena za ndani ya nchi yalipimwa, ambapo matatu, sawa na asilimia 13 ya magari yaliyopimwa yalikutwa na mafuta yenye ubora hafifu.

Hatua madhubuti za kupima mafuta zimesababisha pia kupungua kwa matumizi ya mafuta ya taa toka lita milioni 30 hadi milioni 18 kwa mwezi, na kuporomoka zaidi hadi lita milioni 10 kwa mwezi baada ya serikali kuweka tozo katika mafuta ya taa mwezi Julai 2011.

Mpango wa kuweka vinasaba umeongeza ubora wa mafuta na makusanyo ya kodi serikalini. Taarifa za awali zinaonyesha kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la uagizaji wa mafuta ya dizeli na ya petroli, ambapo petroli imefikia lita milioni 46 toka lita milioni 34.5 kwa mwezi na dizeli kufikia lita 91.5 milioni toka lita milioni 69kwa mwezi.

Ingawa baadhai ya wadau wanapinga uwekaji vinasaba kwa kuwa eti uchakachuaji wa mafuta umepungua baada ya kuongezeka kwa bei ya mafuta ya taa, EWURA itaendelea tu na mpango wake wa uwekaji vinasaba.

Sababu kuu ni kwamba, baada ya kubanwa kwenye uchakachuaji, wafanya biashara wasi waaminifu wanatafuta mafuta yaendayo nje, yaani transit fuel, ambayo kimsingi hayalipiwi kodi, ili wayachanganye nay ale wanayoyauza kwenye visima. Hali hii inachochea kwanza ushindani usio wa haki, pili inaikosesha serikali mapato yake halali kwenye kodi.

MATUKIO KATIKA PICHA

Wakurugenzi wa bodi ya EWURA wakipata maelezo kutoka kwa ofisa wa kampuni ya Symbion, walipotembelea mitambo ya kuzalisha umeme wa dharura jijini Dar es Salaam mwezi Septemba 2011.

Gari ikiwekwa gesi asilia kwenye kituo cha kuuzia gesi huku Mkurugenzi wa Bodi ya EWURA, Bw. Nicholaus Mbwanji (kulia) na Mkurugenzi wa EWURA wa Gesi Asilia Mhandisi Charles Omujuni wakijadili jambo na ofisa wa kituo hicho jijini Dar es Salaam mwishoni mwa mwaka 2011.

MATUKIO KATIKA PICHA

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Gerson Lwenge (wa pili kushoto), Katibu Mkuu, Mhandisi Christopher Sai (wa tatu kushoto) na Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Bashir Mrindoko, wakipewa maelezo na Meneja Ufundi wa EWURA wa Maji, Mhandisi Exaud Fataeli, wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya uhuru, Dar es Salaam, Mwezi Oktoba 2011.

Mdau wa sekta ya petroli akizungumza kwenye uzinduzi wa Kamati ya Ufundi ya Mfumo wa Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja, mwezi Septemba 2011.

MATUKIO KATIKA PICHA

Wakurugenzi wa Bodi ya EWURA, wakiwa kwenye mkutano wa mashauriano kuhusu upatikanaji wa umeme wa dharura na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Mhandisi William Mhando (wa tatu kulia), kwenye makao makuu ya shirika hilo mwishoni mwa mwaka 2011.

Wakurugenzi wa Bodi ya EWURA wakikagua utekelezaji wa mpango wa umeme wa dharura kwenye mitambo ya Aggreko Ubungo, Dar es Salaam mwishoni mwa mwaka 2011.

TANZIA

Bw. Sirili Massay

Bw. Robert Nyirenda

Ni kwa masikitiko makubwa kwamba EWURA imepoteza watumishi wake wawili kati ya waanzilishi wake ambao walijitolea nguvu zao na maisha yao kuifikisha taasisi hii iwe hapa ilipo—Sirili Massay na Robert Nyirenda.

Bw. Sirili, ambaye ndiyo kwanza alikuwa amemaliza mkataba wake wa utumishi na EWURA kama Mkurugenzi wa Bidhaa za petrol Agosti 2011, alifariki dunia asubuhi ya Oktoba 13 2011 kwenye hospitali ya Regency, Dar es Salaam.

Katika salaam zake za rambirambi kwa menejimenti na wafanyakazi wa EWURA, mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi Bw. Simon Sayore alisema: "Nimepokea kwa mshtuko na simanzi kubwa taarifa za kuhuzunisha za kifo cha mwenzetu na rafiki yetu Sirili Massay. Sirili amekuwa mtumishi aliyejitolea kuitumikia EWURA toka ilipoanzishwa hadi alipostaafu hivi karibuni. Ninaamini sote tutamkumbuka kwa ukweli na urafiki na ari yake katika kazi. Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, napenda kutuma salamu za rambirambi kwa mke wa Sirili na familia yake, na kwa wafanyakazi wote wa EWURA, na tunaiombea familia Baraka za Mwenyezi Mungu na uongozi wake wakati huu wa kipindi hiki kigumu cha kuomboleza kuondokea na mpendwa wao."

Hata hivyo, alipokuwa akistaafu, Bw. Massay alielezea kuridhika kwake na taasisi aliyokuwa anaiacha nyuma. Kwenye barua pepe aliyokuwa amewaandikia wale aliowaacha, aliandika: "ama kwa hakika nitaikumbuka EWURA. Hata hivyo, nina hakika ninachowaachia ni moja ya kati ya taassisi thabiti za udhibiti ambayo nimesaidia kuijenga katika miaka yake mitano ya kwanza. Nina imani kubwa na watu mahiri ambao tumewaajiri katika muda huo. Mna menejimenti makini na yenye moyo wa kujituma kazi, na bodi ya wakurugenzi yenye nguvu. Sina hakika nitakuwa wapi baada ya hapa, lakini mkataba wangu na EWURA umefikia ukingoni na inabidi niendelee mbele."

Bw. Nyirenda alifariki tarehe 18 Desemba 2011 katika hospitali ya Burhani, Dar es Salaam. Hadi kifo chake, alikuwa akifanya kazi katika mamlaka kama Mkuu wa Madereva, akiwajibika kumwendesha Mkurugenzi Mkuu. Akiwa mwenye macho ya upole wa babu asiyependa kuwaudhi watoto wake, Bw. Nyirenda alikuwa makini, mfanyakazi hodari ambaye alifanya juhudi bila kuchoka kuhakikisha kuwa alitoa huduma bora kabisa kwa mamlaka. Miezi michache kabla ya kifo chake, aliandika makala inayohusu maisha yake kwa ajili ya jarida hili, makala ambayo hata hivyo hakuwa ameimaliza.

Katika makala hiyo, Bw. Nyirenda anasema anapanga kufanya kazi kwenye shamba lake la mpunga la ekari 20 baada ya kustaafu. Kama mkakati wa kifamilia, anaandika: "...kuhakikisha kuwa binti yangu kitinda mimba anasoma na kukamilisha masomo ya chuo kikuu ambako yuko mwaka wa kwanza."

MWENYEZI MUNGU AWEKE ROHO ZAO MAHALI PEMA PEPONI,
AMINA.

ewura

Energy and Water Utilities Regulatory Authority



EWURA regulates:
Electricity, Petroleum, Gas and Water Services

Our Vision
Quality, affordable and sustainable energy and water services for all.

Our Mission
To champion the delivery of energy and water services through world class regulation for the enhancement of the welfare of the Tanzanian society.

Our Duties
- Promoting effective competition and economic efficiency
- Protecting the interests of consumers
- Protecting the financial stability of efficient suppliers
- Promoting the availability of regulated services to all consumers including low income, rural and disadvantaged consumers
- Taking into account the need to protect and preserve the environment when performing its functions
- Enhancing public knowledge, awareness and understanding of the regulated sectors including rights and obligations of consumers and regulated suppliers, ways in which complaints and disputes may be initiated and resolved and the duties, functions and activities of the Authority.

Our Functions
- Issue, review and cancel licences initiating establishment of standards for goods and services
- Establish standards for terms and conditions of supply of goods and services
- Regulate rates and charges
- Make rules
- Monitor the performance of regulated sectors in relations to levels of investment, availability quality and standards of services, cost of services and efficiency of production and distribution of services. Facilitate the resolution of complaints and disputes.

6th Floor, Harbour View Towers, Samora Avenue, P.O. Box 72175, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 212 3850/3/4/5, Fax: +255 22 212 3860/51524778, Email: info@ewura.go.tz
Website: www.ewura.go.tz